



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



MKOA WA GEITA:

S.L.P. 139
GEITA.

Tafadhali unapojibu taja:

Kumb. Na. GDC/M10/10/VOL III/158

02/07/2024

KWA WATUMISHI WOTE,
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,
S. L.P 139,
GEITA.


**YAH: TAARIFA YA KUENZA MATUMIZI YA NAMBA ZA URAIA (NIN) KATIKA
UTAMBUZI WA WANACHAMA WA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Wilaya ya Geita imepokea barua kutoka Ofisi ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) yenye Kumb Na.DA.174/219/01/117 ya Tarehe 18 Juni, 2024 kuhusu mada tajwa hapo juu.
3. Kufuatia Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) kuunganisha mifumo yake na mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).Mfuko umeboresha utaratibu wa utambuzi wa wanufaika wake kupitia namba zao za Uraia (**National Identification Number – NIN**).
4. Hivi karibuni Mfuko ulianza kuwatambulisha wanachama kutoka kundi la wanafunzi waliofikisha umri wa miaka 18 ambao tayari wana namba za Uraia na walishaziwasilisha NHIF kwa ajili ya kuunganishwa na taarifa zao za Uanachama wa NHIF.
5. Kufuatia mafanikio hayo, Mfuko umepanga kutekeleza kwa wanufaika wake wote waliofikisha umri wa miaka 18 ambao tayari wana namba zao za Uraia na walishaziwasilisha NHIF kwa ajili ya kuunganishwa na taarifa zao za uanachama wa NHIF.
6. Kwa barua hii, Mnataarifiwa kuwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2024 wanachama na Wategemezi waliofikisha umri wa miaka 18 ambao wana namba za NIN na walishaziwasilisha NHIF wataweza kuzitumia kupata matibabu katika vituo vyote vilivyoandikishwa na Mfuko nchini.
7. Matumizi ya Vitambulisho vya NHIF kwa wanufaika ambao hawajafikisha umri wa miaka 18 au ambao hawana NIN wala hawajaziwasilisha NHIF yataendelea kama kawaida.
8. Wanachama waliofikisha umri wa miaka 18 watakojiandikisha kuanzia tarehe 1 Julai,2024 hawatatengenezewa vitambulisho bali watatakiwa kuwasilisha Fomu za uanachama zikiwa na NIN ili ziunganishwe na taarifa zao kabla ya kuzitumia vituoni kupata huduma.

Barua pepe: ded@geitadc.go.tz, Simu Na: 028-25200610, Nukushi Na:028-2520003

Nawatakia utekelezaji mwema.



Karia R. Magaro
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA